Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
## CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021 **KISWAHILI**

(Kwa Watahiniwa Walio na Wasiokuwa Shuleni)

MUDA: Saa 3 — 1 Novemba 2000 MCHANA

**Maelekezo**

1. Jibu maswali MANANE (8) tu: Maswali MANNE (4) kutoka sehemu A na maswali YOTE ya sehemu B.
2. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
3. Andika Namba Yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi

0021

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A: FASIHI

### Kifungu (i) FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 1 au la 2.

1. Eleza tofauti ya kitendawili na methali, kisha toa mifano miwili miwili ili kuthibitisha tofauti hizo.

AU

2. Fafanua muundo wa hadithi za fasihi simulizi kwa kutumia mfano wa hadithi moja unayoifahamu.

## FASIHI – ANDISHI

### Kifungu (ii) USHAIRI

Jibu swali la 3 au la 4.

**VITABU**

Diwani ya Mloka ------------- C. Mloka (B.P.)

Diwani ya Ustadh ----------- A. Andanenga (B.P.)

Malenga Wapya ------------- TAKILUKI (DUP)

3. "Wasanii ni askari wa haki za wanyonge na silaha zao ni kalamu na karatasi"

   Jadili ukweli wa hoja hiyo kwa kutumia washairi wawili kati ya hao waliotajwa.

**AU**

4. Jadili muundo wa kazi za washairi wawili kati ya hao waliotajwa.

### Kifungu (iii) RIWAYA

Jibu swali la 5 au la 6.

**VITABU**

Hiba ya Wivu -------------------------- Z. Mwanga (R.P.)

Kusadikika ------------------------------ S. Robert (Nelson)

Zawadi ya Ushindi --------------------- B. Mtobwa (R.P.)

5. "Mara nyingi riwaya zinatoa changamoto kwa vijana". Jadili kauli hiyo kwa kutumia riwaya mbili zilizotajwa.

AU

6. Jadili utofauti na ufanano wa wahusika wawili kati ya Rusia, Farida na Karama.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Kifungu cha (iv) TAMTHILIYA
Jibu swali la 7 au la 8.

**VITABU**

Hawala ya Fedha -------- A. Lihamba (DUP)

Mfalme Juha -------------- F. Topan (DUP)

Ngoswe – Penzi Kitovu cha Uzembe ------- E Semzaba (E.S.C)

7. "Biashara yoyote haramu haisaidii maendeleo ya jamii". Jadili kauli hiyo kwa kutumia tamthiliya mbili zilizotajwa.

**AU**

8. Toa sababu za kifani zilizowafanya watunzi wawili wa tamthiliya hizo kuzipa majina hayo.

## SEHEMU B: LUGHA

Jibu maswali yote.

9. UFAHAMU

Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata:

Mpenda cha bure boza, tenaje ni baradhuli,
Tamaaye humponza, huzidi kuwa jahili,
Vya bure humwongoza, kwa wengine ajidhili,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Jaribu kuyachunguza, utaiona dalili,
Daliliye inaviza, taufanya namba mbili,
Namba mbili hupoteza, na kupata mushikeli
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Cha bure kitakuponza, ukamshike kipili,
Maneno yangu sikiza, ujifanye fadhalali,
Sasa ninakuongoza, mola chukua kubuli,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Afadhali kukufunza, kwa maneno ya adili,
Jaribu kujichecheza, tena uwe na akili,
Sizidi kujizoweza, nakuasa tafadhali,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Bure kweli hulemaza, tena ina sumu kali,
Epuka vinaumiza, sana vyaleta ajali,
Kooni takukwaruza, ijapo vina samli,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Si kitu cha kuendekeza, falau kuwa asali,
Cha bure kimepooza, ijapo embe kwa wali,
Kiache kina mafunza, hata kitiwe achali,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Wenye hekima hupuza, kuona kitu <u>dhalili</u>,
Na hufanywa kimeoza, kinamfaa tumbili,
Waungwana hukibeza, kwao hakistahili,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Chombo kinachopendeza, pato la jasho halali,
Hutakwamwa ukimeza, lau kama ni ugali,
Na mwisho utamaliza, kuumizwa ni muhali
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Cha wizi ni cha muhonyo, pato hilo siyo mali,
Ndio mlango wa kiza, geuka siukabili,
Utalingia Gereza, jumbo lisilo kandili,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

Tamaa yakandamiza, maneno yangu kubali,
Jambo linalochukiza, mwendo huo ubadili,
Ni kitu cha kuduwaa, moyowee siusabili,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari.

**MASWALI**

(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa shairi hili.

(b) Ubeti wa tano unatufahamisha nini?

(c) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.

(d) Watu gani wanashutumiwa katika shairi hili?

(e) Shairi hili linashabihiana na methali ipi kimaudhui?

10. Andika insha yenye maneno 250 kuhusu moja ya mada zifuatazo:

(a) Madhara ya ajira kwa watoto
(b) Unyanyasaji wa kijinsia
(c) Malumbano ya kidini
(d) Hata aruke vipi kipungu hafikii mbingu.

11. Tumia mzizi wa kitenzi – imb – kuunyambulisha katika hali zifuatazo kwa kupigia mstari kisababisho hicho:

(a) Hali ya urejeshi.
(b) Hali ya kuelekeza ya uyakinishi
(c) Hali ya ukanushi nafsi ya tatu umoja
(d) Hali ya kutendewa
(e) Hali ya kutendeka.

12. Tunga sentensi kuonesha matumizi ya "ku" kwa kupigia hiyo "ku" mstari kama

(a) kinominisho (kitenzi kuwa nomino)
(b) kusaidia shina la kitenzi la silabi moja kubeba mofimu ya wakati.
(c) kuonesha mtendwa nafsi ya pili umoja.
(d) kuunda mzizi wa kitenzi.
(e) Kuonesha mofimu ya wakati

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org